

22B-Aina Za Madd Zinazohusiana Na Maddutw-twabiy'iy (Alif Saba Na Madd Nyenginezo)

Aina za Madd zinazohusiana na مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) ni:

أَلْفَاتُ السَّبْعِ Alifaatus-Sab-'iy - Alif Saba

Hukmu ya مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inayopatikana katika maneno saba pekee ya Qur-aan, hutekelezwa pale anaposimamia tu msomaji. Ama akiendelea kisomo, hukmu ya مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inabatilishwa.

Na hizi zinajulikana kwa jina la أَلْفَاتُ السَّبْعِ (Alifaatus-Sab-'iy - Alif Saba) na alama yake ni kiduara cha umbo la yai juu yake.

Imetajwa katika Qur-aan	Suwhrah Aayah	Neno
Mara kadhaa		أَنَا
Pekee	Al-Kahf: 38	لَنَكْنَأَ
Pekee	Al-Ahzaab: 10	الظُّنُونَأَ
Pekee	Al-Hazaab: 66	الرَّسُولَأَ
Pekee	Al-Ahzaab: 67	السَّبِيلَأَ
Pekee	Al-Insaan: 4	سَلَسِلَأَ
Pekee	Al-Insaan: 15 na 16	قَوَارِيرَأَ

Mfano: Katika kauli ya Allaah (سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى):

إِذْ جَاءُوكُم مِّن فَوْقِكُمْ وَمِنْ أَسْفَلَ مِنكُمْ وَإِذْ زَاغَتِ الْأَبْصَارُ وَبَلَغَتِ الْقُلُوبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّونَ
بِاللَّهِ الظُّنُونًا ﴿١٠١﴾ هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُونَ ...

Aksimama msomaji mwisho wa Aayah katika neno la الظُّنُونًا atasoma:

... wa idh-zaaghatil-abswaaru wabalaghatil-quluwbul-hanaajira
watadhwunnuwana biLLaahidhw-dhwunuwnaa. Hunaalikab-tuliyal-
muuminuwna....

Bonyeza usikilize

Lakini akiunganisha na neno linalofuatia katika Aayah ya pili yake atasoma:

...wa idh-zaaghatil-abswaaru wabalaghatil-quluwbul-hanaajira
watadhwunnuwana biLLaahidhw-dhwunuwnan-hunaalikab-tuliyal-
muuminuwna....

مَدُّ الطَّبِيعِي (Maddutw-Twabiy'iy) Nyenginezo Ni:

- i. مَدُّ الصَّلَاةِ الصُّغْرَى - Maddusw-Swillatis-Sughraa
- ii. مَدُّ الْعَوَظِ - Maddul-'Iwadhw
- iii. مَدُّ الْبَدَلِ - Maddul-Badl
- iv. مَدُّ التَّمْكِينِ - Maddut-Tamkiyn
- v. أَلْفَاتِ حَيِّ طَهْرٍ - Alifaatu Hayyun Twahr